

**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**SHULE YA SEKONDARI MPUNYULE
S.L.P 82,
KILWA-MASOKO
11/12/2019
Simu 0784313002
0718784874**

Kumb Na.MPSS/UT/2019/01

Jina la mwanafunzi _____

S.L.P 160

KILWA MASOKO.

**YAH: MAAGIZO YAKUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MPUNYULE KATA YA MANDAWA
WILAYA YA KILWA MKOA WA LINDI**

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mpunyule ambayo ipo kata ya mandawa halmashauri ya Kilwa. Muhula wa kwanza wa masomo utanza tar 06/01/2020, mwisho wa kuripoti shuleni ni tar 15/01/2020 na baada ya hapo mwanafunzi hatapokelewa na hatua za kisheria zitachukuliwa kwa mzazi. Kutakuwa na kozi maalumu ya kiingereza na itaendeshwa kwa kipindi cha wiki sita za mwanzo hivyo wanafunzi wote wanatakiwa wawahi kuripoti shuleni.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Sare ya shule

a) WAVULANA

- Suruali mbili za kaki
- mashati mawili meupe ya mikono mifupi
- viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili
- soksi nyeusi jozi mbili
- mkanda mweusi
- Tshirt za shule rangi ya bluu(form six) zenye nembo ya shule zinapatikana shuleni kwa Tsh. 13,000/=

b) WASICHANA

- sketi mbili za rangi ya kijani kibichi zinazofunika magoti (kwa waislamu ziwe ndefu za kufunika soksi)
- mashati mawili meupe (kwa waislamu nusu kanzu mikono mirefu mbili zishuke mpaka juu ya magoti na zisibane)
- hijabu (juba) mbili nyeupe za duara na isiwe na mapambo (kwa waislamu tu)
- viatu vyeusi jozi mbili VISIVYO NA KISIGINO KIREFU, visiwe BAJAJI

- Soksi nyeupe jozi mbili ndefu.
- Tshirt za shule rangi ya bluu(form six) zenye nembo ya shule zinapatikana shuleni kwa Tsh. 13,000/=

2.2 MENGINEYO

- Daftari kumi na mbili (kaunta buku), kalamu,penseli,rula na mkebe wa hesabu.
- Matibabu itakuwa ni jukumu la mzazi mwenyewe ikitokea mtoto ataumwa.
- Hosteli kwa wanafunzi wa kike inapatikana kadri utakavyowahi.
- Mwanafunzi aje na jembe aina ya ngwamba lenye mpini, panga na kwanja.
- Aje na Tsh. 2000/= kwa ajili ya faili la kutunzia mitihani yake.
- Aje na Kamusi (dictionary) kwa ajili ya kujifunzia Kingereza.

2.3 Chakula

Chakula cha mchana na uji wa asubuhi vitachangiwa na mzazi ambapo unatakiwa kuleta mahitaji yote ya robo muhula kama ifuatavyo÷

- Unga sembe kilo 23
- Maharage kilo 9
- Mchele kilo 4
- Vitunguu kilo 1
- Sukari kilo 2
- Mafuta ya kupikia kilo 1
- Chumvi kilo 1
- Fedha ya mpishi Tsh.7500/= kwa miezi mitatu

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu yenye dhamana ya elimu nchini na wizara ya ofisi ya raisi TAMISEMI, utumishi na utawala bora yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi kama ifuatavyo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahusiano mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni jambo la lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (evining preparation) ni muhimu.
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa ni jambo la lazima.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule ni jambo la lazima
- g) Kuvaa sare ya shule katika hali ya unadhifu wakati wote unapotakiwa ni jambo la lazima
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ni jambo la lazima na
- i) Kutunza mali za umma ni jambo la lazima.

3.1 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kukusababisha Kufukuzwa Ama Kusimamishwa Shule

- i Wizi
- ii Uasherati na ushoga
- iii Ubakaji
- iv Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kuberi, na kadhalika.
- v Kupigana au kupiga
- vi Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- vii Kudharau bendera ya taifa
- viii Kuwa mjamzito ama kusababisha mimba
- ix Kuoja au kuolewa
- x Kutoa mimba
- xi Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- xii Kukataa adhabu kwa makusudi
- xiii Kuwa na simu ya mkononi

ANGALIZO

Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia,bangili,pete,mkufu,herein,kishaufu,kusuka nywele,kunyoa kipara, kunyoa fasheni yeyote,kutia rangi kucha kutumia dawa za kubadili ngozi rangi na mambo mengine yote yasiyo na maadili ya Kitanzania.

4.0 Mambo Mengine Muhimu Yanayopaswa Kukamilishwa Na Kuwasilishwa Shuleni Na Mwanafunzi

- a) Medical Examination Form Ambayo Itajazwa Na Mganga Mkuu Wa Hospitali Ya Serikali. Fomu Hii Itakabidhiwa Kwa Mkuu Wa Shule Mara Utakaporipoti Shuleni. (Itaambatanishwa Kwenye Kurasa Za Nyuma)
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali Soma Kwa Makini Maelezo/Maagizo Haya Na Uyatekeleze Kikamilifu

NB: fomu hii ijazwe kabla ya kuripoti shuleni ili kupunguza usumbufu.

KARIBU SHULE YA SEKONDARI MPUNYULE

.....

**RASULI H MCHARO
MKUU WA SHULE**

**SHULE YA SEKONDARI MPUNYULE
TAARIFA MAALUMU KUHUSU MWANAFUNZI MPYA**

SEHEMU A

Jina kamili (kwa herufi kubwa) _____

Tarehe ya kuzaliwa _____

Kabila _____ dini _____

Anuani ya nyumbani _____

Kijiji unachotoka _____ Kata _____

Tarafa _____ Wilaya _____ Mkoa _____

SEHEMU B.

Jina la baba..... hai/amefariki.....

Kazi ya baba _____ namba ya simu _____

Jina la mama _____ hai/amefariki _____

Kazi ya mama _____ namba ya simu _____

Taarifa za ndugu kufuata umri (kaka na dada wa mwanafunzi)

| namba | Jina La Ndugu | Kiwango Cha Elimu | Anuani Yake |
|-------|---------------|-------------------|-------------|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |

SEHEMU C: MICHEZO AMA AINA YA SANAA ANAYOPENDA

| Jina la mchezo au sanaa | Shule au mahali | Tangu mwaka | Mpaka mwaka |
|-------------------------|-----------------|-------------|-------------|
| | | | |
| | | | |

SEHEMU D: Kazi Yeyote Ya Uongozi Uliyowahi Kufanya

| Madaraka au kazi | Shule au mahali | Toka mwaka | Mpaka mwaka |
|------------------|-----------------|------------|-------------|
| | | | |

Ninaahidi kuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo

Sahihi ya mwanafunzi _____

Sahihi ya mzazi/mlezi _____

Tarehe _____

UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi _____ ninakubali mtoto wangu _____

_____ asome katika shule ya sekondari Mpunyule na nitahakikisha namtimizia mahitaji muhimu mwanangu wakati wote atakapokuwa anasoma hapo shuleni na nitahakikisha yafuatayo,

- a) Atakuwa hana ruhusa ya kwenda katika nyumba za wageni, maeneo ya ulevi na kwenye miziki nje na utaratibu wa shule.
- b) Ninaahidi kumpatia vifaa vyote vinavyohitajika na ninathibitisha atakuwa na mahali pakulala muda wote mpaka amalize masomo yake.
- c) Ninaahidi kumleta shuleni kwa wakati uliopangwa bila kumchelewesha ili nafasi yake isije ikachukuliwa na wengine wa chaguo la pili
- d) Mwanangu akiwa shuleni alelewe katika dini ya _____
- e) Anuani yangu _____
- f) Sahihi yangu mimi mzazi/mlezi _____
- g) Sahihi ya mwanafunzi _____

Tarehe _____

Naambatanisha fomu ya hospitali.

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

SHULE YA SEKONDARI MPUNYULE

S.L.P 82,

KILWA-MASOKO.

To the medical Officer

.....
.....

SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Name of studentform year

I shall be very grateful if kindly the examination to the above mentioned student, and send a report regarding his/her health condition for his/her suitability in undertaking studies.

1. X-ray
2. Urine
3. Tuberculosis
4. Pregnancy
5. Stool

Preliminary information (by the student before the doctor)

| | Diseases | Yes | No | Disease | Yes | No |
|--|--------------|-----|----|--------------------|-----|----|
| | Tuberculosis | | | Heart problem | | |
| | Pneumonia | | | Kidney and urinary | | |
| | Asthma | | | Malaria | | |
| | Epilepsy | | | Serious accident | | |
| | Skin disease | | | Diabetes | | |
| | Vision | | | STD's | | |